# Nafasi ya Fasihi ya Watoto katika Ukuzaji wa Mshikamano wa Kitaifa

*Muge Tecla*
*Chuo Kikuu Cha Moi, Kenya*

**Ikisiri**

**Fasihi ya watoto ni aina ya sanaa ambayo imeandaliwa kwa ajili ya watoto. Fasihi hii inaweza kuwa imetungwa na kuandikwa na mtu mzima au mtoto, na hulenga watoto kama hadhira teule. Sanaa hii huhusisha tanzu nyingi ambazo zinawapa watoto nafasi za utendaji. Fasihi ya watoto ina tanzu anuai nazo ni nyimbo na ushairi, michezo ya kuigiza, hadithi, mchongoano na misemo miongoni mwa nyingine. Wakati wa utendaji, watoto hujumuika na wenzao ili kutekeleza utanzu wowote. Wanapojumuika pamoja, watoto huonyesha ushirikiano wao kupitia ugawanyaji wa majukumu, vifaa vya kuchezea, uongozi wa nyimbo na kuwakinga wenzao dhidi ya madhara yoyote. Wanapofanya hivyo, watoto hukuza umoja na mshikamano baina yao. Wakati wa kuimba kwa mfano, watoto huimba kwa zamu ili kila mmoja ahisi kuthaminiwa na wenzake. Ni kwa msingi huu ndipo makala haya yanapambanua nafasi ya fasihi ya watoto katika ukuzaji na uendelezaji wa mshikamano wa kitaifa na utangamano.**

**Maneno Muhimu:** Fasihi Ya Watoto, Mshikamano, Utangamano

## Utangulizi

Makala haya yanahusu uchambuzi wa uamilifu wa fasihi ya watoto katika ukuzaji wa umoja na utangamano wa kitaifa. Fasihi ya watoto ni sanaa maalum inayoandikwa kwa ajili ya watoto (Wamitila, 2003). Ngugi (2011) anashadidia hoja hiyo kwa kudai kuwa fasihi ya watoto ni dhana inayorejelea utunzi unaowalenga watoto pekee. Kulingana na wataalamu hao wawili, fasihi ya watoto huweza kuwa hadithi, ushairi, visakale au drama ambazo zimetungwa kwa ajili wa watoto na vijana. Wataalamu hao wanaendeleza kuwa fasihi ya watoto lazima ijikite katika mambo matatu makuu: mhusika mkuu lazima awe mtoto, dhamira iwahusu watoto na lugha sahili itumiwe kuendeleza msuko. Bakize (2014) anawaunga mkono kwa kuhoji kuwa fasihi ya watoto inalenga hadhira ya kitoto. Kwa ujumla, fasihi ya watoto ni aina ya sanaa inayotumia lugha kupitisha ujumbe kwa hadhira iliyo chini ya miaka 18.

Kutokana na maelezo hayo, kazi za watoto ni lazima ziwe katika hali inayofaa watoto kwa kila namna ili waweze kuimarishwa katika udogo wao. Mti uliokuzwa vizuri hunawiri vyema na hustahimili hali zote. Mtoto ni kama mti na kwa hivyo ni jukumu la walezi wao kuwanyosha wakiwa na umri mdogo. Ni muhimu kwa walimu wa fasihi ya watoto kuchukua sehemu yao katika maisha ya watoto walio mikononi mwao.

**Fasihi ya Watoto na Utangamano wa Kitaifa**

Kwa mujibu wa Akoleit (1990), utangamano wa kitaifa unahusu uhusiano mzuri wa kijamii uliojengwa juu ya mhimili mkuu wa amani. Hoja hii inatuelekeza katika kuzingatia kile ambacho kinaweza kukuza na kudumisha umoja miongoni mwa wanajamii. Umoja huo hukuzwa tangu utotoni. Ili mti unawiri vyema, shartiimwagiliwe maji na kuwekwa virutubishi vya kutosha. Mti kama huo utastahimili changamoto za kiangazi na utaendelea kukua itakikanavyo. Vilevile, mtoto anayepata mahitaji ya kutosha, hatakuwa na wakati mgumu katika kukabiliana na changamoto za utu uzima.

Mtoto aliyekuzwa vyema hutangamana na wenzake bila matatizo mengi. Umoja na mshikamano huu haujali lugha au kabila. Hii ni kwa sababu watoto hujua tu kuwa wenzao ni watoto kama wao bila kuzingatia iwapo wanatoka jamii tajiri au maskini, wanasema lugha tofauti au sawa na yao, ni weupe au weusi miongoni mwa mambo mengine. Utangamano wa aina hii hukuza umoja na uwiano miongoni mwa watoto na wanajamii kwa ujumla.

**Kazi za Watoto katika Kukuza Umoja**

Kama asemavyo Silau (2013), nyimbo zina dhima nyingi katika maisha ya watoto. Anasema kuwa nyimbo ni muhimu katika ukuzaji na uimarishaji waa malezi katika jamii. Wanapoimba nyimbo zao, watoto hushirikiana na wenzao ili uimbaji uweze kuwa na ladha na kupata maana. Tofauti na watu wazima wanaoweza kuimba pekee yao na kutafakari maneneno ya nyimbo, watoto huimba na wenzao katika hali ya ushirikiano na utendaji ili nyimbo husika zipate maana. Ushirikiano huo unaleta umoja miongoni mwa watoto. Aidha, maudhui katika nyimbo hizo huonya, hurekebisha tabia na kutunuku wenye tabia njema.

Watoto huendelea kukua kimwili, kisaikolojia na kisosholojia na wao hutegemea watu wazima kuwaelekeza. Maelekezi hayo huweza kupitishwa kwa njia nyingi na hata kupitia nyimbo. Wakati wanapokuwa, watoto wanajaribu kuuelewa ulimwengu wa nje wanamokulia na unaopanuka kila kukicha. Wanapofanya hivyo, watoto hujaribu kuelewa hisia zao ambazo hazijaimarika bali bado zinayumbayumba. Hisia hizo hudhibitiwa na utangamano ambao unakuza umoja miongoni mwao. Nyimbo zilizo na maudhui ya umoja na mshikamano hukuza tabia njema miongoni mwa watoto kwa sababu wao hutaka kudumisha uhusiano kupitia kutowakosea wenzao. Wanapofanya hivyo, hisia za upendo na amani hujengeka ndani yao. Wanapowajali wenzao katika uimbaji kwa mfano kuwapa nafasi ya kuanzisha wimbo, watoto wanadhihirisha umoja

kati yao. Mmoja anapoumia, watoto humhurumia na kujitolea kumsaidia. Kujitolea huko ni kukuza hisia tofautitofauti katika maisha na humsaidia mtoto kukubali hali fulani na kuwa tayari kukabiliana na hali nyinginezo zitakazoibuka maishani.

Wanasaikolojia wanasema kuwa wazazi na wadau wote wanapaswa kuelewa mahitaji ya kimsingi ya watoto. Salehi (2011) anahoji kuwa hisia za watoto ni dhaifu na mahitaji yao ni mengi. Mahitaji hayo yakipuuzwa, watoto watakumbana na changamoto nyingi maishani ambazo zitawashinda kukabiliana nazo. Ni muhimu kutaja kuwa, ili kujenga mielekeo chanya kwa watoto, waelekezi wanafaa kuelewa mahitaji yao ya kimsingi. Hivyo basi, ni bora kushughulikia mahitaji ya mtoto kwa njia inayofaa. Mbali na mahitaji ya kimwili, watoto hupenda Skudadisi ulimwengu unaowazingira ambao ni wa kiuhalisia na kisaikolojia.

Licha ya watoto kufurahia sana ulimwengu wa kifantasia, mara nyingi hupenda kujua uhalisia wa mambo yanayotukia katika maisha yao, ya wenzao naya wanajamii kwa ujumla. Udadisi huo unawapa fursa ya kukua kiakili na jambo hilo huwapelekea kujiandaa katika upanuaji wa mawazo na kukaribisha utu uzima. Ukuaji huo unaweza kutekelezwa iwapo watoto watapewa nafasi ya kufanya mambo ya utoto katika miaka ya utoto. Wakati wa utekelezaji huo, watoto hushirikiana kupitia: Ugawanaji wa majukumu, uzingatiaji wa wadogo wao, kugawana vifaa vya kuchezea, kuimba kwa zamu, kuwashughulikia wenzao wanapoumia, kutoa kinga dhidi ya madhara yoyote pamoja na na kuzawadi na kuadhibu. Katika sehemu ifuatayo nimejadili vipengele hivi kwa kina.

**Umoja Kupitia Ugawaji wa Majukumu**

Watoto wanapotagusana katika michezo yao hujipata katika hali inayowalazimu kugawana majukumu. Wanalazimika kufanya hivyo ili kuhakikisha kuwa kila mmoja anashirikishwa. Walio na umri mkubwa huchukuwa uongozi na kuhakikisha kuwa kila mmoja amezingatiwa. Iwapo kikundi kina watoto wa viwango tofautitofauti kiumri, ni wazi kwamba majukumu yatagawanywa kulingana na umri. Wale wadogo kabisa watapewa majukumu mepesi na waliowapiku kwa umri watajipa majukumu mazito kidogo. Mfano mzuri ni katika mchezo wa kuigiza wa 'Chababa' na 'Chamama'. Ni kawaida kwa watoto wawili ambao huonekana bingwa katika mazungumzo na maamuzi na pia ni wakubwa kiumri kuchukua nafasi hizo mbili. Ni lazima hao wawili wawe wa jinsia tofauti na kinachofurahisha ni kwamba watoto hujipa wenyewe nafasi hizo za kijinsia bila kuelekezwa na watu wazima.

Katika mchezo huo wa 'Chababa' na 'Chamama', wale wanaochukua nafasi za wazazi huchukua uongozi wa kugawa majukumu kwa walio wadogo wao. Nao wadogo huwatii "wazazi" wao bila pingamizi lolote. Wanapoambiwa wapeleke'ng'ombe' malishoni au kulea 'mtoto', wao hutii na kuhakikisha kuwa wanatekeleza mambo yote katika ushirikiano. Uongozi na utiifu hujenga uhusiano mwema miongoni mwa watoto hao na huwaandaa katika utu uzima. Uhusiano huo ndio unaowapelekea kukuza umoja na utangamano mzuri kati yao. Katika mkabala huo, watoto hao watakapokuwa watu wazima wataendeleza umoja huo hata katika kiwango cha taifa.

**Umoja na Upendo Kupitia Kuwajali Wadogo Wao**

Ni kawaida kwa watoto kuwajali na kuwashughulikia wenzao. Mara nyingi wanapokutana katika shughuli za kujifurahisha, watoto wakubwa huwazingatia sana walio na umri mdogo zaidi. Kwa mfano mtoto aliye mdogo kuliko wengine hushughulikiwa na karibu kila mmoja. Utagundua kuwa atapewa vitu vingi kwa mfano matunda, vifaa vya kuchezea na hata kuonyeshwa upendo mwingi. Mtoto huyo atabebwa mgongoni na karibu kila mmoja hupigania kumlea. Iwapo atalia, wengine watang’ang’ania kumbembeza na kumliwaza. Ni ishara kuwa watoto wanadhihirisha umoja na upendo kupitia kuwashughulikia wadogo wao.

Wakati wa kugawana ‘chakula’ kwa mfano, watoto wengine hukubali kutulia ili walio wadogo zaidi washughulikiwe kwanza. Baadaye walio wakubwa kidogo hushughulikiwa kabla ya walio wakubwa kabisa. Shughuli hizi zote zinawapa watoto nafasi ya kujitayarisha katika maisha ya baadaye na kuwa tayari kukabiliana na changamoto za ujana na utu uzima. Hali ya kuwajali wadogo wao na kuwashughulikia katika kuwapa mahitaji yao ina uwezo mkubwa wa kukuza maadili mema miongoni mwa watoto na kuwapa nafasi ya kujenga uhusiano mwema. Watoto ni kielelezo kizuri kwa jamii na iwapo watu wazima wangekuwa na hali kama ya watoto,(ya kuwashughulikia wenzao), watu wangeishi kwa amani, upendo na umoja.

**Umoja Kupitia Kuimba kwa Zamu**

Kipera cha nyimbo ndicho kipana zaidi katika fasihi ya watoto. Nyimbo hutekeleza majukumu makubwa katika maisha ya watoto. Kama ilivyo kwa watu wazima, nyimbo za watoto huliwaza, huonya, husifu, huburudisha, hufundisha na kufurahisha. Ni nadra sana kuwapata watoto wakiimba hali wamenuna. Hii ni kwa sababu nyimbo zao nyingi ni za furaha. Ni kawaida kwa mtoto kuadhibiwa na mamaye kisha baada ya kulia na kutoroka, hurudi kama anaimba wimbo wa kumsifu au kumfurahisha mamaye. Kwa mfano katika wimbo:

**1.** Nani penda mimi – mama penda mimi ×2
Nani penda mama – mimi penda mama ×2
Ma….aaa.ma, peeeeenda mi,
Miiiiimi, peeeeenda ma,
Mimi mimi penda ma
Mama mama penda mi
Mimi mama pendana.

Katika hali ya kawaida, mtoto ataimba wimbo huu huku akimwangalia au kumshikashika mamaye mgongoni. Mtoto atakuwa amesahau kuwa aliyemwadhibu ni mama na atakuwa anapigania tu upendo wa mama. Hii inadhihirisha kuwa wao ni watu wasiopenda vikwazo bali furaha kila wakati.

Nyimbo huchukua nafasi kubwa katika kukuza ubunifu wa mtoto. Utampata mtoto akiimba kwa sauti ambayo umeisikia lakini maneno ni tofauti. Wao hupenda kuingiza maneno yao wenyewe kwa nyimbo ili kuelezea kilicho akilini na wanachofikiria kwa wakati huo. Kupitia kwa nyimbo, watoto hupata nafasi ya kujifunza mengi hasa kupitia

maudhui ya wimbo husika. Wakati wa uimbaji, anayeongoza wimbo huwataja wenzake kwa zamu ili waweze kuendeleza uimbaji. Mfano:

**2.** (*akizunguka mviringo*) Sungura amelala na jicho moja wazi ×2
Wee sungura we, wee sungura we
Tandalitata tata ×2
Taa (*akimshika mwenzake kichwa ili aendeleze wimbo)*

Pia, wakati wa uimbaji,anayeongoza wimbo ana uwezo wa kuwataja watakaoingia ndani ya mviringo ili kufanya utendaji. Kiongozi huyo anaimba na anapowataja majina wanaotakiwa kucheza, wanaotajwa hujitokeza moja kwa moja ili kutimiza matakwa ya wimbo husika. Wao huingia uwanjani kwa maringo na kufanya wanachoambiwa na kiongozi wa wimbo. Baada ya kucheza au kufanya walichokusudiwa waliotajwa huondoka uwanjani ili kuwaachia wenzao zamu. Watoto hufanya hivyo ili kuhakikisha kuwa kila mmoja amejumuishwa. Ni kwa msingi huu ndipo tunasema kuwa nyimbo za watoto hukuza na kuendeleza mshikamano na umoja miongoni mwao. Mfano mzuri ni katika Wimbo ‘La la laa’:

**3.** La la laa – la ×2
Kosi ingia ndani – la
Na rafiki yako – la
Ujiringeringe – la
Ujikunekune – la
Ucheze shomwana na utoke nje, aee mama
Walushele kamatumbezi, onyango skotee skotee
Waa (*waliondani ya mviringo kuingia na wengine wanapishwa ndani)*

Upokezanaji zamu ni mbinu inayokuza ushirikiano miongoni mwa watoto. Wao hufanya hivyo bila mapendeleo kwani kila mmoja hupata nafasi ya kushiriki katika kucheza. Ushirikiano huo hujitokeza tu bila kulazimishwa kwa sababu kazi za watoto zinahitaji kutendwa kwa pamoja ili ziridhishe na kufurahisha na pia kuleta maana. Watoto huwatii sana wenzao na utawapata wakingojea zamu zao bila kusumbua kabla ya kutajwa. Hii ni dhihirisho kuwa watoto ni kielelezo kizuri cha kuigwa na watu wazima ambao mara nyingi hung’ang’ania vitu hata visivyo muhimu katika maisha. Raha hupatikana katika upeanaji wa nafasi ili kila mmoja ahisi kushirikishwa na kukubalika na wenzake.

### Umoja Kupitia Kuadhibu na Kutuza

Licha ya umri wao mdogo, watoto wanaelewa kuwa ulimwengu tuliomo una mambo mawili tu, kutuza na kuadhibu. Wanajua kwamba anayetenda kitu kizuri hutuzwa na anayetenda kibaya huadhibiwa. Hii hutokana na kile wanachopitia tangu wanapozaliwa. Labda, adhabu ya kwanza apatayo mtoto kutoka kwa mamaye ni wakati anamnyonyesha. Iwapo atauma titi la mamake, atachunwa kidogo ili ajue si vyema kufanya hivyo. Na atakaporudia mara ya pili atapewa kichuno kikali kidogo kuliko ya kwanza na kuanzia hapo atajua kuwa ni jambo baya linaloandamana na adhabu. Kama asemavyo Cass (1967), masimulizi ya watoto yanahitaji kuonyesha hali mbili: ya uovu

na wema lakini wema ushinde uovu. Anashadidia kuwa watenda wema watuzwe na watendao maovu waadhibiwe.

Kando na adhabu, tuzo la kwanza apatalo mtoto hutokea wakati analia na licha ya kutoelewa anachosema mamake, atajua kuwa anaponyamaza hupata tuzo la kupendwa na mama. Pia wakati analishwa na mama, mtoto huzungumziwa ili amaliza chakula. Punde tu mama anapohisi kuwa mtoto ameshiba, humpongeza kwa kumshikashika usoni na kumfanya acheke. Mtoto huyo anapoendelea kukua, huamini kuwa akila vizuri mamake atampenda na huko ni kutuzwa.

Ruthiri (2012), anapendekeza kuwa mtoto anatakiwa kupata hisia za kutosha kumfanya ahisi kuwa duniani kuna mchanganyiko wa machungu na matamu. Anaendelea kusema kuwa mtoto anapaswa kukumbana na hali zote. Hali hizi ziwe za kuzua uchungu kwa kiasi kidogo na hali za furaha kwa kiwango fulani. Madai hayo yanaashiria kuwa kila mtoto anapaswa kushiriki masikitiko ya wengine ili aelewe ubia wa hisia za binadamu. Kutokana na ukweli huo, ni vyema kwa wadau wote washirikiane ili kuhakikisha kuwa watoto wanapata nafasi ya kutagusana na uhalisia wa maisha.

Vivyo hivyo, katika michezo yao, watoto huamini kuwa jambo lolote linalotendwa linalipwa kuwili, kuadhibiwaau kutuzwa. Mfano mzuri ni wakati mtoto anajaribu kuwa mchokozi au kumchapa mwingine. Wenzake watamkemea na iwapo kuna wakubwa kumshinda ataadhibiwa vikali. Iwapo ni mkubwa kuwapiku wenzake, ataambiwa kuwa atashtakiwa kwa wazazi na hakika ripoti itawafikia wazazi. Kuadhibu na kuzawadi ni njia mojawapo ya kuwaelekeza watoto kuwa na tabia njema katika utoto wao ili watakapokuwa watu wazima, waweze kukabiliana na changamoto za maisha. Ni mbinu ya kukuza heshima na ushirikiano miongoni mwao.

## Hitimisho

Katika makala haya, imebainika kuwa fasihi ya watoto ina nafasi muhimu sana katika ukuzaji wa mshikamano wa kitaifa. Fasihi hiyo kupitia hadithi, nyimbo, michezo ya kuigiza pamoja na vipera vingine inaweza kutumika katika kuwaandaa watoto kuwa watu wa kutegemewa na ambao wanapenda umoja, amani na utangamano. Hili litawezekana tu iwapo watoto watapatiwa nafasi ya kuwa watoto na kuelekezwa kwa upendo na hata wazazi wao kuwa kielelezo bora. Fasihi ya watoto basi ni njia mojawapo inayoweza kutumika katika kuwaelekeza watoto kushika adabu na kuwaheshimu wenzao. Aidha, ni njia maalum ya kupitisha maadili kwa watoto na kuwapa nafasi ya kudadisi ulimwengu unaowazingira kupitia mtagusano wao wa kila siku.

Katika mkabala huo basi, watunzi wa kazi za watoto wanapaswa kuzingatia uteuzi mzuri wa mada za kazi zitakazowaelekeza watoto kuwa na tabia njema yenye adabu na itakayoleta furaha katika maisha yao ya baadaye.Ni vyema kuelewa kuwa watoto hushika na kudhamini sana kile wanachosikia na kukutana nacho kwa mara ya kwanza. Wazazi na wadau wote wakitoa malezi mema pamoja na mahitaji yote ya kitoto kwa watoto wao, nafasi nzuri ya kukuza talanta kwa watoto itapatikana.

**Marejeleo**

Akoleit, J. (1990). Response and Criticism in Children's Literature in Kenya. The Case of Barbar Kimenye. Tasnifu ya uzamili (haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Bakize, L. H. (2014). *Utangulizi wa Fasihi ya Watoto*. Dar es Salaam: Moccony Printing Press.

Cass, J. E. (1967). *Literature and the Young Child.* City Longman Group Limited

Ngugi, P. (2011). *Language and Literacy Education: The state of Children's Literature in Kenya.*Berlin: Lambert Academic Publishing.

Ruthiri, M. K. (2012). Tathmini ya Ufaafu wa Vitabu vya Kusoma kwa Madarasa ya 5 na 6 katika Shule za Msingi: Mifano ya Waandishi Wanne. Tasnifu ya uzamili (haijachapishwa); Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Salehi, A. (2011).*Foundations and Principles of Psychological content of Children's Books.* Makala yaliyowasilishwa katika kongamano la fasihi ya watoto. Bongokok. Psrcentre.org./images/extraimages/36pdf. 08.08.2018

Silau, A. (2013). Tathmini kuhusu dhima za nyimbo katika kukuza na kuimarisha malezi katika kabila la Wakaguru. Tasnifu ya uzamili (haijachapishwa), Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi Focus Books.